



DAILY NEWS PAGE 19

# *Ferry fish market supply low due to poor fishing tech *

By JAMES KAMALA

FISHERMEN at Ferry fish market have said poor technology is the major cause for fluctuation of fish supply particularly on rainy or windy weather season.

Vice-chairman of the Dar es Salaam small scale fishers' association (UWAWADA), Mr Saleh Msaen said in Dar es Salaam yesterday that high tech fishing gear may help them to go fishing into deep water even in bad weather.

The 'Daily News' survey established that fresh fish prices at Ferry fish market have gone up exponentially with fishers not fearing the outbreak of coronavirus in their work but blaming the down pouring seasonal rains amid low technology used for fish catch.

Beginning this week, a twenty-kilogram bucket of sardine will be sold at up to 45/-from 30/-, previously. Other types of small size fish have seen the price shoot to 55/-from the normal price of 35/-for a 20-kgm bucket.

"The main challenge faced is that we can't catch fish at deeper level of the sea for we are incapable of casting nets deeply," he said.

He said that the hard situation was caused by the fact the ongoing seasonal rains are increasing the amount of cold water into the sea through river tributaries, which causes the fish to swim deeper into the sea in search of saline water.

"This makes our catch more difficulty as we don't have modern technology to support deepest sea fishing; We end up into losses which jeopardises our business and livelihood," he said.

He said that a boat, which sails with up to 12 fishermen, is forced to dock back to the beach after 11 days as working and basic needs runs off.

"After 10 days in the sea, they (Fishers) need fuel for boat engines, food and ice bars to store few catches," Insisted Msean.

# Minister nullifies cattle auction ban over Covid-19

By DEUS NGOWI


THE Deputy Minister for Livestock and Fisheries, Mr Abdallah Ulega has nullified the order by Monduli District Commissioner (DC), to ban cattle auction market at that the verdict was arrived due to the fact that the government has banned mass gatherings as they are partly a means for Covid-19 patients to infect others.

He was of the opinion that the market attracts cattle

Scanned by CamScanner

ta Kusini, Nelson Mandela

MWANANCHI UK 10



HAJI MTUMWA

# Ajira ya kupaa samaki si nzuri, inaharibu watoto

Zanzibar ni miongoni mwa visiwa vilivyojaliwa neema ya bahari nzuri na yenye kuvutia.

Wananchi wake pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) wamekuwa wakiitumia Bahari ya Hindi katika shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na maendeleo.

Miongoni mwa shughuli ambazo hutumika kupitia bahari hiyo ni pamoja na uvuvi, kilimo cha mwani, utalii na shughuli nyingine zenye kuingiza kipato kwa jamii na Taifa.

Licha ya bahari kutumika kwa matumizi mbalimbali, matumizi makuu ni uvuvi ambao hutoa fursa kubwa hasa kwa wananchi wanaoishi maeneo ya karibu na bahari kuvua na kuuza mazao ya baharini.

Hii ni moja ya fursa ambayo imekuwa ikichangamkiwa kwa kasi hasa na vijana wanaoishi pembezoni mwa bahari kutokana na utendaji kazi wake, hauhitaji elimu ya shule, chuo au utaalamu ambao upatikanaji wake huwa mgumu kwa wanyonge.

Vijana wengi wamekuwa wakinufaika na matumizi ya bahari, baadhi yao kupitia uvuvi.

Kutokana na hali hiyo, wengine hawatamani hata kazi nyingine za kuwaingizia kipato.

Hakuna asiyefahamu kwamba kazi ya uvuvi imegawika katika maeneo mbalimbali, wapo wavuvi, madalali wa kuuza samaki, wanunuzi pamoja na wahudumu wa mwisho ambao ni waparaji samaki baada ya wanunuzi kununua.

Lakini katika makala haya nazungumzia kazi ya kupaa samaki ambayo hufanywa na watoto ambao wengi wao walitakiwa wawe shule.

Kwa kuwa kazi hiyo huonekana ni kazi ya mwisho kabisa katika sekta ya uvuvi na haina malipo makubwa, hivyo visiwani Zanzibar watoto walio chini ya miaka 18, ndio wahusika wakuu wa kupaa samaki.

Kutokana na malipo ya kazi hiyo kuwa madogo, mara nyingi huachiwa watoto waifanye.

Hata hivyo, baadhi ya watoto hufanya kazi hiyo huku wazazi au walezi wao wakitambua, lakini wanawaacha pasipo kujua kuwa walipaswa wawe shule.

Wazazi au walezi ndio huwa wasimamizi wakuu wa watoto hao kwa kuhakikisha kuwa wanapata kazi nyingi za kupaa samaki ili wapate pesa za matumizi.

Licha ya wazazi hao kuona wanachofanya kuwa ni sahihi kwa maslahi yao dhidi ya watoto hao, lakini ukweli ni kwamba kufanya hivyo ni kuwadumaza watoto kiakili.

Mbali na kuwadumaza pia wanakuwa wanawaandalia watoto maisha mabaya hapo baadaye kwa kuwa baadhi yao wamekatisha masomo.

Pia, watoto hao wanakuwa hawana malezi bora kwa kuwa wanakutana na watu wa aina tofauti hivyo heshima kwao huwa si kitu cha muhimu.

Ni mara nyingi tumekuwa tukisikia malalamiko ya walimu hasa kwa shule zilizopo karibu na bahari, wakidai kuwa utoro kwa watoto wa maeneo hayo umekuwa ni mambo ya kawaida.

Pia, wanasema wazazi huwa hawana wasiwasi na watoto kwa kutohudhuria masomo, licha ya juhudi kubwa kuchukuliwa na walimu kama kuitisha vikao mara kwa mara ili kujadili mustakabali mzuri wa utoaji wa elimu kwa watoto.

Ifahamike kwamba licha ya wazazi kuona kufanya hivyo ni kuwapenda watoto au kuwapa mbinu za kutafuta pesa mapema, lakini njia hiyo ni kuwapotosha watoto na kuwaandalia mazingira mabaya katika maisha yao ya baadaye.

> **Tumekuwa tukisikia malalamiko ya walimu hasa kwa shule zilizopo karibu na bahari, wakidai kuna utoro kwa watoto wa maeneo hayo.**

Umefika wakati sasa kwa wazazi, taasisi mbalimbali za wanaharakati pamoja na Serikali kwa ujumla kushirikiana kwa pamoja katika kulifanyia kazi suala la watoto kutoshiriki kazi ya uparaji wa samaki ili kuona watoto hao wanaandaliwa vyema kuwa viongozi wazuri wa familia, au serikali hapo baadaye.

Licha ya taasisi mbalimbali kikiwamo Chama cha Waandishi wa Habari za Maendeleo Zanzibar (Wahamaza) na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef) kufanya kazi kubwa ya kutoa elimu juu ya umuhimu wa elimu na malezi bora kwa watoto, lakini bado wazazi wana haki kubwa ya kuona watoto wao wanaishi katika mazingira bora.

Tunaamini hilo linawezekana iwapo kila mmoja atatambua umuhimu wa kuwatunza na kuwalea watoto katika makuzi bora hasa ya kielimu.

Ni jukumu la kila mmoja kumlea vyema mtoto, ili baadaye afurahie matunda ya kuwa na wataalamu wenye sifa nzuri kutoka ndani ya nchi badala ya kuwa na wataalamu kutoka nje ya nchi.

Scanned by CamScanner

# Hatima ya Halima Mdee kujulikana Aprili 28

**Na REHEMA MOHAMED**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu inatarajia Aprili 28, mwaka huu kutoa uamuzi wa iwapo Mbunge wa Kawe, Halima Mdee (CHADEMA) kama ana kesi ya kujibu au la.

Uamuzi huo unatarajiwa kutolewa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, baada ya upande wa Jamhuri katika kesi hiyo ya uchochezi, kufunga ushahidi wao kwa kuita mashahidi watatu.

Hakimu Simba alipanga tarehe hiyo jana wakati shauri hilo lilipopelekwa kwa ajili ya kutolewa uamuzi huo.

Awali, Wakili wa Serikali, Silvia Mitanto alidai kesi ilipelekwa kwa kutolewa uamuzi wa iwapo mshitakiwa ana kesi ya kujibu ama la, lakini hayupo mahakamani.

Hata hivyo, mdhamini wa Mdee, Faris Lupomo alidai mshitakiwa anaumwa mkono na kuwasilisha barua kutoka Hospitali ya Aga Khan ikionesha ni mgonjwa.

**Lengo>>**Kuhakikisha minada ya mifugo inaendelea kufanya kazi

# Serikali yaagiza elimu dhidi ya corona kutolewa kwenye minada ya mifugo

**NA LILIAN JOEL,** ARUSHA

SERIKALI imewaagiza viongozi waliopo kwenye mikoa ya wafugaji nchini, kutofunga minada ya mifugo, badala yake watoe elimu kwa wafanyabiashara kuendelea na majukumu yao bila mikusanyiko.

Pia, wametakiwa watoe elimu ya kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa corona kwa kunawa mikono kwa maji tiririka.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Naibu Waziri wa Uvuvi na Mifugo, Abdallah Ulega, alipotembelea soko la kimataifa la mifugo, lililopo mpakani mwa Tanzania na Kenya, wilayani Longido na eneo la mnada wa mifugo lililopo eneo la Meserani wilayani Monduli.

Alisema ni lazima biashara na shughuli za kiuchumi ziendelee ili serikali ipate mapato na kuwezesha familia za kifugaji kupata mahitaji muhimu kwa sababu hazina kipato kingine.

"Hatuwezi kufunga minada hii kwa sababu maisha ya Watanzania walio wengi huishi kwa kutafuta mlo wa kila siku, hivyo kuzuia minada ni sawa na kutaka wafe kwa njaa, sasa hili serikali tumelitafakari kwa kina na tumeona haifai kuifunga minada," alisema.

Aliwasisitiza wafanyabiashara wote kwenye minada hiyo kuchukua tahadhari kwa kunawa mikono kwa kutumia maji tiririka muda wote wanapokuwa eneo la mnada na kupunguza msongamano wa watu eneo la minada isiyo ya lazima.

Ninachosisitiza hapa kwenye minada hii wawepo tu wale wanaouza mifugo na wanaonunua, lakini mkishauziana tu ondokeni mara moja mnadani na sitaki muweke mikusanyiko na katika hili naomba mlizingatie," alisema.

Aidha, alipongeza minada hiyo aliyotembelea kwa kukuta wamechukua tahadhari kwa kuweka vitakasa mikono na maji tiririka na kuhakikisha kila anayeingia eneo hilo ananawa mikono yake.

Ulega aliagiza pia kwa yeyote atakayekaidi kunawa mikono kwa hiari achukuliwe hatua kali ili kunusuru afya yake na watu wanaomzunguka. Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frack Mwaisumbe, aliishukuru serikali kuruhusu wananchi wake kuendelea na minada ya mifugo, sababu ni sehemu ya maisha yao.

"Mwanzoni ugonjwa huu ulivyoingia tulizuia kidogo biashara hii na kuzua taharuki kwa wafugaji wetu, lakini baadae Waziri Mkuu Kassimu Majaliwa aliwasiliana na viongozi wenzake wa nchi jirani ya Kenya na kuturuhusu kuendelea na minada yetu na kweli wanakuja wakenya wengi katika soko letu la kimataifa la hapa mpakani Namanga kununua mifugo," alisema.

Kuhusu tahadhari, Mwaisumbe alisema wanachukua zote ili kuhakikisha kila anayeingia katika eneo hilo anakuwa salama dhidi ya ugonjwa huo.

Wafanyabiashara wa mifugo nchini, Solomon Laizer na Lomnyaki Mollel, walishukuru kuruhusiwa kuuza mifugo yao na kuiomba serikali kuweka vipima joto kwenye minada yao ili kila atakayeingia apimwe na atakayebainika kuwa na shida asiruhusiwe kuingia mnadani.

Scanned by CamScanner

# *Wafugaji 231 Sikonge wapewa elimu ya ufugaji wa kisasa*

**Na Allan Ntana, Sikonge**

■■JUMLA ya wafugaji wa asili 231 wilayani Sikonge Mkoani Tabora wamefundishwa njia na mbinu bora za ufugaji wa kisasa ili kuongeza tija katika mazao ya mifugo wanayozalisha ikiwemo kumiliki ardhi.

Akiongea na gazeti hili juzi Ofisa Mifugo na Uvuvi wilayani humo Mipawa Majebele alisema kuwa mkakati huo umelenga kuboresha mifugo na ufugaji na kuinua maisha ya wafugaji.

Mbali na elimu alisema pia wamehamasishwa kumiliki ardhi kwa kupatiwa hati na kutumia hati hiyo na rasilimali walizonazo kukopea fedha benki ili kuboresha shughuli zao, na kuongeza kuwa hii itasaidia kupunguza migogoro isiyo na tija baina yao na wakulima.

Aidha katika kuhakikisha mifugo yote inakuwa salama katika wilaya hiyo alisema jumla ya ng'ombe 105,385 sawa na asilimia 52 ya ng'ombe wote wamechanjwa chanjo ya CBP huku mbwa 250 wakipata chanjo ya kichaa katika kata zote 20.

Kwa upande wa wafuga samaki Majebele alifafanua kuwa wametoa elimu ya ufugaji bora na wa kisasa kwa jumla ya wafugaji 63na wamefanikiwa kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu kutoka asilimia 25 hadi 20.

Aidha kutokana na doria waliyofanya katika maeneo mbali mbali ya uvuvi alisema kuwa wamefanikiwa kukamata nyavu haramu 46 ambapo nyavu 33 zilichomwa moto na 13 ziliwasilishwa ofisi ya mifugo na uvuvi kwa ajili ya kutolea elimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya hiyo Martha Luleka alisema kuwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi 2019 halmashauri hiyo imejenga mnada wa kisasa katika kata ya Mpombwe kwa gharama ya sh mil 30.

Aidha katika kuhakikisha sekta hiyo ya mifugo na uvuvi inaongeza mapato ya ndani ya halmashauri hiyo Martha alisema kuwa wanatarajia kuanzia ujenzi wa minada mingine 2 ya kisasa katika kata za Sikonge na Kiloli na tayari sh mil 30 zimetolewa kwa ajili ya kuanza kazi hiyo.

Alibainisha kuwa maboresho makubwa ya miundombinu ya ufugaji na wafugaji yaliyofanywa na halmashauri hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi na wataendelea kufanya maboresho makubwa katika sekta zote.

*DC awa... kidole w... wazem...

**Na Mwand...**

■ ■ MKU... Tunduru mk... Mtatiro, am... wa vijiji, mi... tarafa kuwa... kutokana na... watazamaji... kushindwa... kutatua m... wananchi k... kazi.

Alisema, ... a Serikali, ... sehemu ya... ndiyo war... hatua ya ku... ya wananc... ya utawala... yeyote atal... basi ataku... mwenyew...

Scanned by CamScanner

# Wafugaji watakiwa kuchukua tahadhari ya Corona

**Na Mwandishi Wetu, Arusha**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amewataka wafugaji kuhakikisha wanachukua tahadhari juu ya ugonjwa wa Corona.

Akizungumza na wafugaji mara baada ya kutembelea minada ya mifugo katika Soko la Kimataifa la mifugo lilipo wilayani longido pamoja na mnada wa Meserani wilayani Monduli Mkoa wa Arusha, Ulega alisema tahadhari ni muhimu kuchukuliwa na kuhakikisha wafugaji na wafanyabishara wananawa mikono.

Alisema pindi biashara ya mifugo inapofanyika ni vyema kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, ambapo pia aliwataka wafugaji kurejea majumbani ili kujikinga na ugonjwa huo.

Katika hatua nyingine, Ulega alitembelea Kituo cha Wizara ya Mifugo na Uvuvi kilichopo Namanga na kuzungumza na maofisa wa kituo hicho, ambapo alisema serikali imeruhusu biashara kufanyika kama kawaida, hivyo waisaidie serikali katika eneo hilo.

Alisema ni lazima biashara na shughuli za kiuchumi ziendelee, ili serikali ipate mapato huku familia nazo zipate mahitaji yao muhimu.

"Hatuwezi kufunga minada hii, sababu maisha ya Watanzania walio wengi huishi kwa kutafuta mlo wa kila siku, hivyo kuzuia minada ni sawa na kuataka wafe kwa njaa, sasa hili serikali tumelitafakari kwa kina na tumeona haifai kuifunga minada hii," alisema.

Aliongeza; "Ninachosisitiza hapa kwenye minada hii wawepo tu wale wanaouza mifugo na wanaonunua, lakini mkishauziana ondokeni mara moja mnadani na sitaki muweke mikusanyiko," alisema.

Alipongeza minada hiyo kutokana na tahadhari zilizochukuliwa ambapo ili kudhibiti mikusanyiko, makundi ya wafugaji na wafanyabishara imepungua kwa kiasi kikubwa tangu kulipozuka ugonjwa huo, huku kila anayeingia ananawa mikono kwa maji safi yanayotiririka.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frack Mwaisumbe aliishukuru serikali kuruhusu wananchi wake kuendelea na minada ya mifugo, sababu ni sehemu ya maisha yao huku akieleza wazi kuwa awali mnada huo wa Longido ulifungwa kutokana na kuzua taharuki kubwa kwa wananchi mara baada mgonjwa wa kwanza wa Corona kutangazwa.



# Tabora waomb Jeshi la Polisi kuimarisha dor

**Na Allan Ntana, Tabora**

WAKAZI wa Manispa Tabora wameliomba Jes Polisi kuimarisha doria, ili ku vitendo vya uhalifu vinavyoen kuongezeka katika ma mbalimbali mjini hapa.

Walisema vitendo hivyo vim vikijitokeza mara kwa mara mitaa mbalimbali ambapo wamekuwa wakivamiwa, ku kujeruhiwa na kuibiwa ma pasipo kukamatwa.

Wakizungumza na Majir nyakati tofauti walisema, usalama wao na mali za sasa ni wa mashaka kutok matukio hayo.

Walisema hivi sasa kun

Scanned by CamScanner